

# JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na.DCC/AC.66/1

Tarehe 19/10/2023

## TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia uwepo wa ajira ya Mkatoba kwa nafasi zifuatazo:-

### 1. MHANDISI WA UJENZI (MENEJA WA USIMAMIZI WA MIRADI): NAFASI (1)

#### Sifa za Mwombaji:

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe na Elimu kuanzia Kidato cha Nne/Sita
- Awe na Shahada/Stashahada ya Uzamili ya Uhandisi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na waliosajiliwa na Bodi za Usajili wa fani husika
- Awe na uzoefu usiopungua miaka mitano na kuendelea katika ujenzi na usimamizi miradi

#### Kazi na Majukumu:

- Kufanya kazi za Uhandisi na Usimamizi wa Miradi

### 2. MHANDISI MKADIRIAJI UJENZI (QUANTITY SURVEYOR) NAFASI (1)

#### Sifa za Mwombaji:

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- Awe na Elimu kuanzia Kidato cha nne/sita
- Awe na Shahada/Stashahada ya Uzamili ya Uhandisi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na waliosajiliwa na Bodi za Usajili wa fani husika

**Kazi na Majukumu:**

- Kukusanya taarifa na takwimu kuhusu miradi mbalimbali kuhusu bei za vifaa vya majengo ndani na nje ya nchi
- Kupitia mapendekezo ya miradi (project proposals) mbalimbali

**Maombi yaambatanishwe na:**

- Nakala ya Cheti cha kidato cha Nne/Sila
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Nakala za vyeti vya Taaluma –Shahada/Stashahada ya Juu
- Picha 2 (Passport size)

**Jinsi ya kutuma maombi:**

Barua zote za maombi ya kazi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili na namba za simu za mwombaji, Barua Pepe na zivasilishwe ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 2/11/2023 saa 9.30 alalri.

  
Jomeary M. Satura  
MKURUGENZI WA JIJI

MKURUGENZI WA JIJI  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

**Anuani ya kutuma Maombi:**

Mkurugenzi wa Jiji,

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,

S.L.P 20950,

DAR ES SALAAM.